TANGAZO LA SERIKALI NA. 531 la tarehe 28/6/2024

SHERIA YA MISITU
(SURA YA 323)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 29(1))*

AMRI YA KUTANGAZA MSITU WA HIFADHI KILINGA YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Msitu wa Hifadhi Kilinga ya Mwaka 2024.

Tangazo

2. Eneo la ardhi ya mataji wazi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi Kilinga.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA MANYONI

MSITU WA HIFADHI KILINGA

*Makadirio ya Eneo:* Hekta 10916.44 au Kilometa za Mraba 109.16

Unakopatikana na Mipaka

Eneo lote la ardhi ya mataji wazi awali chini ya Msitu wa Kilinga linalopatikana Wilaya ya Manyoni, Mkoa wa Singida kama lilivyochorwa katika Ramani ya Idara ya Upimaji Jb 2731 ya mwaka 2018 (Skeli 1:25000) iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na lenye mipaka ifuatayo:




Dodoma,
24 Mei, 2024

ANGELLAH JASMINE KAIRUKI,
*Waziri wa Maliasili na Utalii*